



TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO HILI LIMEIDHINISHWA NA MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA)

HATIFUNGANI YA KIJANI YA MIUNDOBINU YA MAJI YA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA (TANGA UWASA)

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) inatoa taarifa kwa umma kwamba Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Tanga UWASA kuuza Hatifungani ya miaka 10 yenye thamani ya shilingi bilioni 53.1 (TZS 53,120,000,000) itakayowezesha kupata fedha za kutekeleza shughuli za ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji na utunzaji wa mazingira.

TAARIFA YA HATIFUNGANI – HATIFUNGANI YA KIJANI YA MIUNDOBINU YA MAJI YA TANGA UWASA

Muhtasari wa taarifa muhimu za Hatifungani hii zimewekwa hapa chini:

Mtoaaji	Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA)
Kiasi	TZS 53,120,000,000 (Shilingi za Kitanzania Billioni Hamsini na Tatu na Milioni Mia Moja na Ishirini)
Riba iliyopangwa (Kuponi)	13.50% kwa mwaka itakayolipwa mara mbili kwa mwaka
Kiwango cha chini	TZS 500,000 (Shilingi za Kitanzania Laki Tano)
Tarehe ya toleo	22 Aprili 2024
Tarehe ya kuiva kwa hatifungani	22 Aprili 2034
Tarehe za malipo ya riba	22 Oktoba na 22 Aprili
Riba ya hatifungani	Asilimia 13.50 kwa mwaka. Riba isiyobadilika itakayolipwa mara mbili kwa mwaka
Muda wa hatifungani	Miaka 10
Kodi	Hatifungani haina kodi ya zuio
Kuorodheshwa DSE	Hatifungani itaorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)

Uwekezaji unafanyika kwa kujaza Fomu ya Maombi inayopatikana kwenye matawi ya Benki ya NBC (National Bank of Commerce Limited), kwa mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam waliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko na Dhamana (CMSA); au kwenye tovuti ya Tanga UWASA www.tangauwasa.go.tz. Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti ya benki ya NBC iliyoainishwa hapo chini:

Akaunti ya malipo

Akaunti ya TZS.

TANGA UWASA BOND	020139000046
------------------	--------------

TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU

	Tukio	Tarehe
1.	Tarehe ya kuidhinishwa Waraka wa Matarajio wa Hatifungani ya Tanga UWASA kutoka CMSA	Jumanne 20 Februari 2024
2.	Tangazo la hatifungani kwa Umma	Alhamisi 22 Februari 2024
3.	Kuanza kupokea maombi ya ununuzi wa hatifungani	Alhamisi 22 Februari 2024
4.	Mwisho wa kupokea maombi ya ununuzi wa hatifungani	Alhamisi 4 Aprili 2024
5.	Kuwasilishwa kwa rejista CSDR	Jumatano 17 Aprili 2024
6.	Mgao kwa wawekezaji	Jumatatu 22 Aprili 2024
7.	Kutangaza matokeo ya mauzo ya hatifungani	Jumanne 23 Aprili 2024
8.	Taarifa ya kupata hatifungani kwa Wawekezaji	Jumanne 23 Aprili 2024
9.	Kulipia hatifungani	Jumatano 24 Aprili 2024
10.	Tarehe ya toleo	Jumatano 24 Aprili 2024
11.	Kuingiza CDS kwenye mfumo wa DSE	Jumatano 24 Aprili 2024
12.	Kuorodheshwa Kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)	Jumanne 30 Aprili 2024
13.	Mwisho wa Hatifungani	Jumatatu 24 Aprili 2024

Wawekezaji wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mtendaji,
Tanga UWASA,
S. L. P 5011,
Tanga,
Tanzania.**